Jitathmini 21.4 (ukurasa wa 120-121)

1. hu-
2. (a) hukiriza, husali, huiva, hunywewa
(b) kiambishi hu-
(c) hu-
3. *Mimi <u>husoma</u> katika Shule ya Heshima. Kila asubuhi, mimi <u>huamka</u> mapema sana. Baada ya kuoga, mimi <u>hupiga</u> mswaki. Baadaye, mimi <u>huvalia</u> sare yangu ya shule na kunywa kiamshakinywa. Baba <u>hunipeleka</u> kwenye stendi kungoja basi la shule. Baada ya kuliabiri, baba <u>huenda</u> kazini. Mimi <u>hupenda</u> kuenda shuleni.*
4. (a), (c), (d)
5. (a) Yaya huosha vyombo vichafu.
(b) Barabara hii huharibiwa na magari mazito.
(c) Mwavuli hutukinga dhidi ya mvua.
(d) Kucha zote ndefu hukatwa.
(e) Masoko yetu husafishwa.
6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina kiambishi hu- cha hali ya mazoea kisha ufanye ulivyoagizwa.
7. Mwasilishie mzazi au mlezi sentensi zako na uhakikishe amezitolea maoni.

ii. Hali timilifu

Jitathmini 21.5 (ukurasa wa 121)

1. -me-
2. (a) imekamilika, wamecheza, imefumwa
(b) kiambishi -me-
(c) -me-
3. *Maisha ya sasa <u>yamerahisishwa</u> sana. Mashine <u>zimevumbuliwa</u> ambazo <u>zimefanya</u> mambo kufanyika kwa urahisi. Uvumbuzi huo <u>umefanya</u> habari kusambaa haraka sana kote duniani. Isitoshe, usafiri baina ya mabara <u>umewezekana</u> kupitia kwa usafiri wa kisasa. Watu pia <u>wameweza</u> kuiga mitindo ya kigeni. Uigaji huu <u>umewezeshwa</u> na teknolojia.*
4. (a), (d), (e)
5. (a) Tajiri amewasaidia mayatima wale.

(b) Mashine zimechanganya mchanga na simiti.
(c) Jengo kubwa limejengwa mjini.
(d) Hoteli hii imeuza chakula kitamu.
(e) Refa amepuliza kipenga.
6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina kiambishi -me- cha hali timilifu kisha ufanye ulivyoagizwa.
7. Mwasilishie mzazi au mlezi sentensi zako na uhakikishe amezitolea maoni.

iii. Hali ya -ki- ya masharti
Jitathmini 21.6 (ukurasa wa 121-122)
1. Wakati wa kuonyesha masharti.
2. (a) (i) **Nikinunua** rinda jipya nitahudhuria sherehe hiyo.
(ii) Kipindi kingine **kikianza** nitaenda kulala.
(iii) Nywele **zikioshwa** zinang'ara.
(iv) Wakimbizi **wakipata** makazi watafurahia.
(v) Sweta **ikishonwa** itavaliwa.
(b) kiambishi -ki-
3. *Darasa letu ni safi sana. kila jioni tukimaliza vipindi tunaokota uchafu wote. Tukifagia sakafu tunaiosha pia. Sakafu ikikauka, tunapanga madawati na kufunga darasa letu. Asubuhi tukifika shuleni, tunahakikisha viatu vyetu ni safi kabla ya kuingia darasani. Tunajua kuwa tukisoma katika mazingira safi, tunatunza afya yetu pia.*
4. (b), (c), (e)
5. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina kiambishi -ki- cha hali ya masharti kisha ufanye ulivyoagizwa.

iv. Hali ya masharti ya -nge-

Jitathmini 21.7 (ukurasa wa 122-123)

1. Inatumika kuonyesha sharti ambalo bado lina uwezekano wa kutimizwa katika wakati uliopo au wakati ujao. Jambo hilo linaweza kutokea ikiwa tu sharti husika litafuatwa.

2.(a) (i) Ningeamka, ningefika
(ii) Wangekamilisha, wangelipwa
(iii) Angemwona, angemkumbatia
(iv) Ungefanya, ungeshinda
(v) Tungefika, tungehudhuria
(b) -nge-
3. Pigia mstari vitenzi hivi: wangetunzwa, wangepata, wangesoma, wangepata, wangekuwa, wangewatibu, wangekuwa, wangelisha
4. (a), (b), (d), (e)
5.(a) Tunga sentensi sahihi.
(b) Fanya zoezi hili na mwenzako.

v. Hali ya masharti ya -ngali-

Jitathmini 21.8 (ukurasa wa 123)

1. Inatumika kuonyesha sharti la wakati uliopita ambalo halikutimizwa, na kwa hivyo matokeo yake hayawezi kubadilika tena (sharti lisilowezekana au lililopitwa na wakati).

2.(a) ningalitembea, mngalisoma, ungalinionya, angalikimbia, wangalicheza

(b) -ngali-

3. Pigia mstari vitenzi hivi:

Ningalijua, ningalimchukulia, ningalipiga, ningaliwaonya, ningaliandika,wangaliusoma, wangaliepuka

4.(a) (a), (b), (c), (e)

5.(a) Tunga sentensi sahihi.

(b) Zingatia matamshi bora unapomsomea mwenzako sentensi zako.

6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye zoezi ulilopewa.

vi. Hali ya -ka- ya kufuatana kwa vitendo

Jitathmini 21.9 (ukurasa wa 123-124)

1. Wakati wa kuonyesha vitendo viwili au zaidi vinatendeka vikifuatana.

2. (a) (i) Mlango ulifunguliwa watu **wakaingia** kwa nyumba.

(ii) Kochi zilishonwa **zikapendeza**.

(iii) Osebe aliosha nguo **akazianika**.

(iv) Viatu vilichafuka **vikapanguswa**.

(v) Biarusi alifika sherehe **ikaanza**.

(b) kiambishi -ka-

3. (a) Wimbo huo uliimbwa <u>ukavuma</u> kila mahali.

(b) Alichemsha maji, <u>akaweka</u> unga kisha <u>akapika</u> sima.

(c) Mechi ilianza, <u>wakacheza</u> na <u>wakashinda</u>.

(d) Ugonjwa ulikurupuka na watu <u>wakapata</u> chanjo.

(e) Kabati ilifunguliwa, dawa <u>ikawekwa</u> ndani kisha <u>ikafungwa</u>.

4. (b), (c), (e)

5. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina kiambishi -ka- ya kufuatana kwa vitendo kisha ufanye ulivyoagizwa.

Wakati uliopita hali ya kuendelea na wakati ujao hali ya kuendelea

Jitathmini 21.10 (ukurasa wa 124)

1. Tunazingatia nyakati na hali mbalimbali katika mawasiliano ili kuleta uwazi, usahihi na mtiririko mzuri wa habari. Nyakati hutusaidia kujua ni lini jambo lilitendeka (wakati uliopita), linatendeka (wakati uliopo), au litatendeka (wakati ujao). Hali nayo hueleza jinsi kitendo kinavyofanyika—ikiwa kinaendelea, kimekamilika, au ni cha masharti. Hii huzuia utata na mchanganyiko wa mawazo wakati wa kuzungumza au kuandika.

2. kiambishi -na-

3.(a) (ii), (iv), (v)

(b)

- Wanafunzi wa<u>na</u>soma.
- Mariamu a<u>na</u>pika viazi.
- Ni<u>na</u>vua samaki.

i. Wakati uliopita hali ya kuendelea

Jitathmini 21.11 (ukurasa wa 124)

1.Kuonyesha tendo lililokuwa likiendelea katika wakati uliopita kauli ilipokuwa ikitolewa.

2. -li-, -na-

3. (a) (i), (iii), (v)

(b)

- Mama <u>alikuwa anapika</u> mboga.
- Pendo <u>alikuwa anaandika</u> insha.
- <u>Tulikuwa tunafua</u> sare zetu.

iii. Wakati ujao hali ya kuendelea

Jitathmini 21.12 (ukurasa wa 125)

1. Kuonyesha kitendo kitakachokuwa kikifanywa wakati kauli itatolewa baadaye.

2. -ta-, -na-

3.(a) (ii), (iii), (iv)

(b)

- Mtoto <u>atakuwa analala</u>.
- Mama <u>atakuwa anaandaa</u> chajio.
- Kiatu <u>kitakuwa kinashonwa</u>.

4. (a) Amani atakuwa anasoma maktabani.

(b) Paka atakuwa anakunywa maziwa.

(c) Mkimbiaji atakuwa anashinda dhahabu.

(d) Nyanya atakuwa anaenda mjini.

(e) Toni atakuwa anaosha vyombo.

iv. Wakati uliopita hali timilifu

Jitathmini 21.13 (ukurasa wa 125)

1. Kuonyesha kitendo kilichokuwa kimekamilika muda mfupi kabla ya kauli kutolewa (katika wakati uliopita).

2. -li-, -me-

3.(a) (i), (ii), (iv), (v)

(b)

- Wanafunzi walikuwa wameandika insha.
- Mgeni alikuwa amewasili.
- Kiatu kilikuwa kimeshonwa.
- Seremala alikuwa ametengeneza meza nyingine.

4. (a) Amani alikuwa amesoma maktabani.

(b) Paka alikuwa amekunywa maziwa.

(c) Mkimbiaji alikuwa ameshinda dhahabu.

(d) Nyanya alikuwa ameenda mjini.

(e) Toni alikuwa ameosha vyombo.

v. Wakati ujao hali timilifu
Jitathmini 21.14 (ukurasa wa 126)

1. Kuonyesha kitendo kinachotarajiwa kuendelea kufanyika wakati kauli itatolewa baadaye.
2. -ta-, -me-
3. (a) (i), (ii), (iv), (v)
(b)

- Mwema atakuwa ameoga.
- Wachezaji watakuwa wamejiandaa.
- Mika atakuwa ameondoa vyombo mezani.
- Fahali atakuwa amepewa chakula na maji.

4. (a) Amani atakuwa amesoma maktabani.
(b) Paka atakuwa amekunywa maziwa.
(c) Mkimbiaji atakuwa ameshinda dhahabu.
(d) Nyanya atakuwa ameenda mjini.
(e) Toni atakuwa ameosha vyombo.

20. Ukanushaji

Ukanushaji kwa kuzingatia nyakati na hali

a. Ukanushaji kwa kuzingatia nyakati

i. Wakati uliopo

Jitathmini 22.1 (ukurasa wa 126)

1. Hali ya kukana kuwa jambo linaloendelea kufanyika wakati kauli inatolewa halifanyiki.

2. Tunakanusha sentensi kwa kuzingatia wakati uliopita, wakati uliopo na wakati ujao.

3. (a) Fundi hajengi nyumba yetu.

(b) Mwanafunzi hasomi kitabu cha hadithi.

(c) Dereva haendeshi gari kwa kasi.

(d) Mama hapiki chakula kitamu.

(e) Mwalimu hasahihishi vitabu vyetu.

4. (a) Utingo hafungi mzigo.

(b) Mtoto hachezi na mwanasesere wake.

(c) Baba hachongi kinyago.

(d) Talo hawalishi mifugo wake.

(e) Wnafunzi hawasafishi darasa.

5. Tunga sentensi sahihi.

ii. Wakati uliopita

Jitathmini 22.2 (ukurasa wa 126-127)

1. Hali ya kupinga kuwa kitendo kilichofanyika wakati uliopita hakikufanyika.

2. Viambishi vya nafsi na vya wakati uliopita.

3(a) Wachezaji hawakufanya mazoezi yao.

(b) Baba hakuezeka paa la nyumba.

(c) Mama hakuchota maji kisimani.

(d) Waziri hakuitembelea shule yetu.

(e) Nyanya hakutusimulia kisa hicho.

4.(a) Mosha hakuchanja kuni.

(b) Sikutuzwa na waziri wa michezo.

(c) Pendo hakusafiri kwenda ng'ambo.

(d) Kiatu changu hakikununuliwa sokoni.

(e) Wanafunzi hawakuenda maktabani.

5. Tunga zentensi sahihi.

iii. Wakati ujao

Jitathmini 22.3 (ukurasa wa 127)

1. Hali ya kupinga kuwa kitendo kinachotarajiwa kutokea baadaye hakitakokea.

2. viambishi vya nafsi na wakati

3.(a) Beka hatasafiri kwenda Ulaya.

(b) Nkirote hatamtembelea nyanya.

(c) Paka hatapewa maziwa.

(d) Wageni hawatafika.

(e) Kisima hakitachimbwa.

4. (a) Baba hataenda kazini.

(b) Kaka hataninunulia kamusi.

(c) Hamali hatabeba mizigo.

(d) Kiranja hatatuongoza.

(e) Jirani hatajenga ukuta kuzunguka nyumba yake.

5. Tunga sentensi sahihi.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

b. Ukanushaji kwa kuzingatia hali

i. Hali ya mazoea

Jitathmini 22.4 (ukurasa wa 127)

1. Kupinga kuwa jambo linalofanyika mara kwa mara halifanyiki.

2. Utazingatia wakati, hali na nafsi.

3.(a) Nyale hakimbii asubuhi.

(b) Mtoto halali alasiri.

(c) Jogoo hawiki alfajiri.

(d) Paka hanywi maziwa.

(e) Yeye hamtembelei nyanyake kila Jumamosi.

4. (a) Baba haendi kazini.

(b) Kaka haninunulii kamusi.

(c) Hamali habebi mizigo.

(d) Kiranja hatuongozi.

(e) Mama haamki mapema.

5. Tunga sentensi sahihi.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

ii. Hali timilifu

Jitathmini 22.5 (ukurasa wa 127-128)

1. Hali ya kupinga kuwa kitendo kilichokamilika muda mfupi tu uliopita hakikutendeka.

2. viambishi vya hali na nafsi

3. (a) Mtoto hajakula.

(b) Godoro halijanunuliwa.

(c) Kiatu hakijaoshwa.

(d) Maji hayajamwagika.

(e) Jua halijatua.

4.(a) Mlango haujafunguka.

(b) Chakula hakijaiva.

(c) Mwalimu hajakuita.

(d) Moto haujawaka.

(e) Wachezaji hawajaondoka uwanjani.

5. Tunga sentensi sahihi.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

iii. Hali ya masharti ya -nge-

Jitathmini 22.6 (ukurasa wa 128)

1. Hali ya kuonyesha kuwa vitendo viwili vilivyotegemeana vilitokea.

2. Hali ya masharti na viambishi vya nafsi

3. (a) Nisingepika nisingekula.

(b) Tusingemngoja tusingechelewa.

(c) Asingekamilisha kazi asingelipwa.

(d) Msingekaidi ushauri wangu msingepata hasara.

(e) Wasingetualika tusingeenda mkutanoni.

4. (a) Msingeanika nguo zisingekauka.

(b) Tusingechimba kisima tusingepata maji.

(c) Mvua isingenyesha nisingepanda mboga.

(d) Wasingemwona ajuza wasingemsaidia kuvuka barabara.

(e) Usingenitembelea nisingefurahi.

5. Tunga sentensi sahihi.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

iv. Hali ya masharti ya -ngali-

Jitathmini 22.7 (ukurasa wa 128-129)

1. Hali ya kuonyesha kuwa vitendo viwili vilivyotegemeana vilitokea.

2. Hali ya masharti na viambishi vya nafsi

3. (a) Nisingaliamka mapema nisingaliwahi sokoni.

(b) Asingalituita tusingalimwona.

(c) Tusingalimchokoza mbwa asingalitukimbiza.

(d) Msingalivunja sheria msingaliadhibiwa.

(e) Wasingalichelewa mkutanoni wasingalikosa hotuba ya chifu.

4. (a) Asingalisoma asingalifaulu.

(b) Tusingalisafiri mapema tusingalifika.

(c) Nisingalienda sokoni nisingalinunua mboga.

(d) Wasingalijitahidi wasingalifanikiwa.

(e) Usingalimwona ajuza usingalimsaidia kuvuka barabara.

5. Tunga sentensi sahihi.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

v. Hali ya -ki- ya masharti

Jitathmini 22.8 (ukurasa wa 129)

1. Hali ya kuonyesha kuwa kitendo kimoja hakiwezi kutimia ikiwa sharti fulani halijatekelezwa.

2. Hali ya masharti na viambishi vya nafsi

3. (a) Nisiposimama sitamwona.

(b) Asipoenda hospitalini hatatibiwa.

(c) Tusipomsaidia hatamaliza kazi yake mapema.

(d) Msipohudhuria mkutano hamtamwona waziri.

(e) Wasipofanya mazoezi ya kutosha hawatashinda wapinzani.

4. (a) Msiposhirikiana hamtafanikiwa.

(b) Tusipoanza safari mapema hatutafika mjini jioni.

(c) Nisiposakura katika mtandao salama sitapata habari hiyo.

(d) Wasipotembea polepole hawatanyeshewa.

(e) Usipomchokoza mbwa hatakuuma.

5. Tunga sentensi sahihi.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

23. Ngeli na upatanisho wa kisarufi

a. Ngeli ya A-WA

Jitathmini 23.1 (ukurasa wa 129-130)

1. mwalimu, mwanafunzi, mlinzi, mtoto, mama

2. mtoto, mtume, chura, mbuzi, mbu

3. (a) Watoto, mama (b) Wafanyakazi (c) Panzi, viwavi, wadudu, wakulima (d) Ng'ombe, mbuzi (e) Dereva, utingo, ajuza

4. a- katika umoja na wa- katika wingi

5. (a) Vijana wanacheza na mtoto anacheka.

(b) Mgeni akiwasili wenyeji watampokea.

(c) Kondoo hawa watapewa nyasi.

(d) Mzee huyu anatumia kifaa cha kidijitali.

(e) Wapishi wameandaa chakula kitamu.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya A-WA.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya A-WA katika mazingira ya nyumbani.

b. Ngeli ya U-I
Jitathmini 23.2 (ukurasa wa 130)

1. mti, mche, mtaro, mpaka, muwa

2. mlango, mwiba, mikoba, mtego, mkungu

3. (a) Mwavuli (b) Miche (c) Mpira, msumari (d) Mkono, miguu (e) Mshipi

4. u- katika umoja na i- katika wingi

5. (a) Msitu huu umejaa miti iliyo na miba.

(b) Mto huu una maji safi.

(c) Mikate ya wanafunzi imeokwa?

(d) Msemo huu unapendwa na watu wengi.

(e) Mikakati ya kuimarisha amani imewekwa.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya U-I.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya U-I katika mazingira ya nyumbani.

c. Ngeli ya I-ZI
Jitathmini 23.3 (ukurasa wa 130-131)

1. nyumba, kalamu, chupa, shule

2. nyumba, kalamu, karamu, ndoo, simu

3. (a) Shule (b) Kalamu, penseli, karatasi (c) Chupa, ndoo (d) Suruali, sweta (e) Kauli

4. i- katika umoja na zi- katika wingi

5. (a) Hadithi ya wanyama iliwafurahisha watoto.

(b) Soksi hizi zilinunuliwa jana.

(c) Tarakilishi hizo zimetengenezwa.

(d) Redio zimezimwa lakini televisheni imewaka.

(e) Pikipiki hii imebeba mteja.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya I-ZI.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya I-ZI katika mazingira ya nyumbani.

d. Ngeli ya I-I
Jitathmini 23.4 (ukurasa wa 131)

1. chai, chumvi, sukari, furaha

2. miwani, mvua, Krismasi, sukari, chai, Kenya, hofu, damu, asali

3. (a) Chumvi (b) Chai, sukari (c) Furaha (d) Miadi(e) Homa

4. i- katika umoja na i- katika wingi

5. (a) Dhahabu ina thamani kubwa.

(b) Hofu iliyotanda imeisha.

(c) Mvua imepusa.

(d) Baridi ikikulemea unafaa uvae sweta.

(e) Mihadarati inaathiri afya ya watumiaji.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya I-I.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya I-I katika mazingira ya nyumbani.

e. Ngeli ya U-ZI
Jitathmini 23.5 (ukurasa wa 131)

1. ukuta, ua, uzi, wembe

2. ufagio, nyuzi, waraka, nyembe, ufa

3. (a) Ukucha (b) Nyaraka (c) Ufunguo (d) Nyuso (e) Ubeti, wimbo

4. u- katika umoja na zi- katika wingi

5. (a) Nyua zitazunguka nyumba yao.

(b) Ufito umekatwa na babu.

(c) Nyuzi hizi zitatumika kushona fulana.

(d) Wavu huu umeraruka.

(e) Nyufa kwenye ukuta zimezibwa.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya U-ZI.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya U-ZI katika mazingira ya nyumbani.

f. Ngeli ya YA-YA

Jitathmini 23.6 (ukurasa wa 132)

1. manukato, maji, mate, marashi

2. mate, makao, mandhari, maji, manukato

3. (a) maziwa, maji (b) Mafuta (c) Makao (d) Maumivu (e) Marashi

4. ya- katika umoja na ya- katika wingi

5. (a) Mazingira yamenadhifishwa.

(b) Maovu yamekomeshwa.

(c) Malipo ya nauli yanafanywa kwa njia ya simu.

(d) Mate yalitudondoka tulipokiona chakula.

(e) Maradhi yamepata tiba.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya YA-YA.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya YA-YA katika mazingira ya nyumbani.

g. Ngeli ya KI-VI

Jitathmini 23.7 (ukurasa wa 132)

1. kiti, kitabu, kijiko, kitanda, kioo

2. chakula, kitanda, kiti, chandarua, kijiji, chuma, kikao

3. (a) kitanda, kiti (b) Chuma, chandarua (c) Vyakula (d) Vioo (e) Kisu, kidole

4. ki- katika umoja na vi- katika wingi

5. (a) Kioo kimepanguswa.

(b) Kitanda kipya kilinunuliwa jana.

(c) Vitabu vyangu vinapendeza.

(d) Kibeti chake kilipatikana jana.

(e) Vitabu vyao vimesahihishwa.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya KI-VI.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya KI-VI katika mazingira ya nyumbani.

h. Ngeli ya LI-YA

Jitathmini 23.8 (ukurasa wa 133)

1. sikio, tumbo, embe, limau

2. tomoko, jicho, gurudumu, gari, mawe, tunda, embe, bega

3. (a) Chenza, chungwa (b) Jicho (c) meno (d) maforosadi (e) Jaketi

4. li- katika umoja na ya- katika wingi

5. (a) Jani la mpera limekauka.

(b) Majembe yao yalinolewa jana.

(c) Jengo hili litakuwa afisi ya waziri.

(d) Chenza limeiva.

(e) Gauni la biarusi linapendeza.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya LI-YA.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya LI-YA katika mazingira ya nyumbani.

i. Ngeli ya U-U

Jitathmini 23.9 (ukurasa wa 133)

1. uji, unga, upendo, ujanja

2. uchoyo, uji

3. (a) uji (b) uzalendo (c) Upendo (d) Uchoyo (e) ujasiri

4. u- katika umoja na u- katika wingi

5. (a) Umeme umeleta maendeleo mengi.

(b) Udenda ulimtoka mtoto alipolala.

(c) Uchovu ulimfanya alale mchana kutwa.

(d) Uvivu umemzuia kufaulu katika mradi wake.

(e) Uigizaji umewaletea watu wengi kipato.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya U-U.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya U-U katika mazingira ya nyumbani.

j. Ngeli ya U-YA

Jitathmini 23.10 (ukurasa wa 134)

1. magonjwa, ulezi, mawele

2. ugonjwa, ubua, ulezi, uovu

3. (a) Magonjwa (b) Movu (c) malezi (d) mawele (e) Ubua

4. u- katika umoja na ya- katika wingi

5. (a) Ugonjwa wake ulitibiwa mapema.

(b) Mabua ya mtama yalipeperushwa na upepo.

(c) Uovu wake ulivuka mipaka.

(d) Mawele ya mama yamemwagika.

(e) Ulezi wake unatumika kama kielelezo.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya U-YA.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya U-YA katika mazingira ya nyumbani.

k. Ngeli ya LI-

Jitathmini 23.11 (ukurasa wa 134)

1. jua, jasho, giza

2. jasho, Agano la Kale, Agano Jipya, jua, giza, vukuto

3. (a) jasho (b) Agano Jipya (c) giza (d) Jua (e) vukuto

4. li- katika umoja na li- katika wingi

5. (a) Jua limewaka mapema mno.

(b) Giza lilitanda usiku.

(c) Jasho lilimtoka alipokuwa anachanja kuni.

(d) Vukuto linasumbua wageni wa eneo hili.

(e) Agano Jipya lilisomwa na mhubiri.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya LI-.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya LI- katika mazingira ya nyumbani.

l. Ngeli ya KU-

Jitathmini 23.12 (ukurasa wa 134-135)

1. kuimba, kucheza, kuandika, kusoma

2. kuimba, kusoma, kucheza, kucheka, kutembea, kupika

3. (a) Kulala (b) Kuimba (c) Kulima (d) Kucheza (e) Kuoga

4. ku- katika umoja na ku- katika wingi

5. (a) Kuimba kwa watoto kunapendeza.

(b) Kuongea na chakula mdomoni kunaudhi.

(c) Kusoma kwetu kumetufaidi.

(d) Kulima kwake kunazingatia masharti ya wataalamu wa kilimo.

(e) Kukimbia kwangu kumeninufaisha.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya KU-.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya KU- katika mazingira ya nyumbani.

m. Ngeli ya PA-KU-MU

Jitathmini 23.13 (ukurasa wa 135)

1. chumbani, darasani, pahali, mahali

2. pahali, mahali, kanisani, shambani, kule, mle, shuleni, nyumbani

3. (a) Nyumbani (b) Chumbani (c) Shambani (d) Shuleni (e) Darasani

4. pa-ku-m katika umoja na pa-ku-m katika wingi

5. (a) Pahali hapa ni pangu.

(b) Kanisani kwetu kunapendeza.

(c) Chumbani mwangu mna kitanda na godoro.

(d) Shimoni mna panya watatu.

(e) Nyumbani kwetu kuna wageni.

6. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina viambishi vifaavyo vya ngeli ya PA-KU-MU.

7. Mtajie mlezi au mlezi wako nomino za ngeli ya PA-KU-MU katika mazingira ya nyumbani.

24. Aina za sentensi

a. Sentensi sahili

Jitathmini 24.1 (ukurasa wa 135-136)

1. Sentensi hizo ziwe na wazo moja tu.

2. (a), (c), (d)

3.

- Vimelea hivi huenea kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.
- Magonjwa haya huambukizwa kwa njia tofauti.
- Vimelea hivi huweza kupitisha kwa hewa.
- Wakati mwingine, vinaweza kusambazwa na wadudu.

4. (a) Magonjwa yamesambaa.

Watoto wamepewa chanjo.

(b) Mafuta yamenunuliwa.

Tutapika kaukau kesho.

(c) Barabara imasakifiwa.

Magari yanapita vyema.

(d) Mechi imeanza.

Mashabiki wanashangilia.

(e) Watu wengi wamehudhuria.

Wote wamefurahia.

5. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina wazo moja tu.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

b. Sentensi ambatano
Jitathmini 24.2 (ukurasa wa 136)

1. (a) Sentensi hizo ziwe sentensi sahili mbili au zaidi zilizounganishwa na kiunganishi.

(b) Sentensi ambatano huwa na mawazo mawili au zaidi ambayo yameunganishwa kwa kiunganishi ilhali sentensi sahili huwa na wazo moja tu.

2. (a), (b), (e)

3.

- Alisonga kando na akaketi chini ya kivuli.
- Aliufungua mkoba wake na akatoa dawa mle ndani.

- Alirusha tembe moja mdomoni kisha akaimeza kwa maji.
- Alipumzika chini ya mti na baada ya muda mfupi alijihisi salama.

4. (a) Ameniomba msamaha na nimemsamehe.

(b) Mtalii alipiga picha na imewafurahisha wengi.

(c) Ndizi zimeiva lakini maembe ni mabichi.

(d) Vioo vimeoshwa ilhali milango imepanguswa.

(e) Sweta maridadi ilishonwa na Sara ataivaa.

5. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zinaunganishwa kwa kiunganishi.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

c. Sentensi changamano
Jitathmini 24.3 (ukurasa wa 136-137)

1. (a) Sentensi hizo ziwe na kirejeshi.

(b) Sentensi ambatano huwa na mawazo mawili au zaidi ambayo yameunganishwa kwa kiunganishi, sentensi sahili huwa na wazo moja tu na sentensi changamano huwa na kirejeshi.

2. (b), (c), (e)

3.

- Mwanafunzi anayemakinika darasani huelewa kinachofunzwa.
- Mwanafunzi ambaye anazingatia nidhamu huwa kipenzi cha watu.
- Ni nani ambaye hapendi mwanafunzi mwenye nidhamu?

4. (a) Kiti kilichovunjika kilitengenezwa./ Kiti ambacho kilivunjika kilitengenezwa.

(b) Moto uliowaka umezimika./ Moto ambao uliwaka umezimika.

(c) Magonjwa yaliyoambukizwa yametibiwa./ Magonjwa ambayo yaliambukizwa yametibiwa.

(d) Sherehe iliyosubiriwa sana imefana./ Sherehe ambayo ilisubiriwa sana imefana.

(e) Ndoo zilizonunuliwa zimejazwa maji./ Ndoo ambazo zilinunuliwa zimejazwa maji.

5. Hakikisha sentensi zako ni sahihi kisarufi na zina kirejeshi.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

d. Sentensi tata
Jitathmini 24.4 (ukurasa wa 137)

1. (a) Sentensi hizo ziwe zinatatanisha kimaana.

(b) Matumizi ya neno lenye maana zaidi ya moja au kutumia baadhi ya kauli zinazoleta dhana zaidi ya moja.

2. (a) (i), (ii), (iv)

(b) (i) Babu alimpa mjukuu wake pesa, Babu alimwadhibu mjukuu wake

(ii) Karori alimpiga kwa sababu ya simu, Karori alitumia simu kumgonga, Karori aliwasiliana naye kupitia kwa simu, Karori alipiga simu kwa niaba yake

(iv) Babu aliona mnyama aitwaye tai, Babu aliona vazi liitwalo tai

3. (a)

- Alipompigia mwanafunzi mwingine, waliona ndege.
- Punde, mwanafunzi mwingine aliungana nao katika mchezo huo.
- Walipomaliza kucheza, walikimbia darasani.
- Mwalimu wa Kiswahili akaingia kuwafunza.

(b)

- ndege – nyuni, chombo cha usafiri kinachopita angani
- Mwingine – ambaye walikuwa wakicheza naye, ambaye hakuwa nao awali
- Walikimbia – walitoroka, walienda haraka
- Mwalimu wa Kiswahili – mwalimu ambaye asili yake ni Uswahilini, mwalimu ambaye hufunza somo hilo

4. Hakikisha sentensi zako zina neno ambalo linaleta utata wa kimaana.

5. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

25. Usemi halisi na usemi wa taarifa

Jitathmini 25.1 (ukurasa wa 137-138)

1. Usemi wa taarifa ni ripoti ya maneno yaliyosemwa au kuandikwa na mtu mwingine.
2. Usemi halisi ni maneno au sentensi inayotoka kinywani mwa mzungumzaji moja kwa moja ilhali usemi wa taarifa ni ripoti ya maneno yaliyosemwa au kuandikwa na mtu mwingine.
3.

- Wakati uliopita hubadilika na kuwa wakati uliopo.
- Alama za uakifishaji kama vile alama za nukuu hutumiwa.
- Kiambishi -nge- hubadilika na kuwa -ta-.

- Nafsi ya tatu hubadilika na kuwa nafsi ya kwanza. Kwa mfano: yeye hubadilika na kuwa mimi.
- Siku hiyo hubadilika na kuwa leo.
- Chake hubadilika na kuwa changu.
- Viwakilishi vionyeshi na vivumishi viashiria vya mbali hubadilika na kuwa vya karibu. Kwa mfano: Hapo au pale hubadilika na kuwa hapa.

4. Fanya zoezi hili na mwenzako.

Katika kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa, nyakati na nafsi hubadilika kama ifuatavyo.

- Nafsi ya kwanza na ya pili hubadilika na kuwa ya tatu.
- Kiambishi -ta- hubadilika na kuwa -nge-.
- Viwakilishi vionyeshi na vivumishi viashiria vya karibu hubadilika na kuwa vya mbali kidoho au vya mbali sana. Kwa mfano: hapa hubadilika na kuwa hapo au pale.
- Leo huwa siku hiyo.
- Jana huwa siku iliyotangulia.
- Sasa huwa wakati huo au ule.
- Kesho huwa siku itakayofuata
- Alama za nukuu, kiulizi na alama ya hisi hazitumiki katika usemi wa taarifa.

5. Shirikiana na mwenzako kujadili kanuni za kubadilisha usemi wa taarifa kuwa usemi halisi. Rejelea majibu ya zoezi la tatu.

6. (a)“Unafaa kutunza vitabu vyako,”mama alimweleza Fatuma.

(b) “Mazingira yenu yanapendeza,” wageni walituambia.
(c) “Vipi wanafunzi wanatupa taka ovyo!” Mwalimu alishangaa.
(d) “Hakikisha umefuata maagizo”, Ogindi alimwambia Kailon.
(e) “Nguo hizi ni nzuri,” baba alisema.

1.

(a) “Je, utaenda shuleni kesho?” mama aliniuliza.
(b) “Njoo hapa haraka!” mwalimu mkuu alimwita Juma.
(c) “Darasa lenu limesafishwa vizuri?” mwalimu aliuliza.
(d) “Tunajenga vyoo vingine,” mwalimu mkuu alisema.
(e) “Toka hapa!” Ngoswe alifoka.

8. (a) Tunga sentensi tano za usemi halisi ukizingatia maadili ya kitaifa. Sentensi ziwe sahihi.

(b) Zibadilishe sentensi ulizozitunga katika nambari ya 8(a) ziwe katika usemi wa taarifa. Sentensi ziwe sahihi.

9. Fanya zoezi hili na mwezako.